



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI



Simu: 255-732980745  
Nukushi: 255 732980745  
Barua Pepe: [ded@misungwidc.go.tz](mailto:ded@misungwidc.go.tz)  
Tovuti: [www.misungwidc.go.tz](http://www.misungwidc.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)  
S.L.P 20,  
**MISUNGWI**

KUMB. NA. MZA/MDC/MMP/D/131/1

14/03/2022

### TANGAZO KWA WANACHI WOTE

#### **YAH: TANGAZO LA KAZI ZA MUDA ZA KUKUSANYA TAARIFA ZA MFUMO WA ANWANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi anawatangazia Wananchi wote kwamba Halmashauri ya Misungwi imetoa Nafasi 110 za ajira ya muda kwa Vijana kwa kazi ya kukusanya taarifa za anwani za Makazi na Postikodi kwa Vijiji 115 na Kata 27 za Halmashauri ya Misungwi.

#### SIFA ZA MWOMBAlJI

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:-

- a) Awe Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na anayeishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.
- b) Awe na umri wa kuanzia miaka **18 hadi 45**.
- c) Awe na Kitambulisho cha NIDA au Namba ya NIDA au Kitambulisho chochote.
- d) Awe na simu janja yenye mfumo wa Adroid ikiwa na uwezo wa kutunza chaji kwa siku nzima na aweze kutumia muda wote wa zoezi.
- e) Asiwe **Mtumishi wa Umma** katika Sekta yoyote.
- f) Awe na barua pepe (e-mail address) na nywila (password).
- g) Awe na Elimu ya Kidato cha Nne na kuendelea (Aambatishe nakala ya cheti cha Elimu).
- h) Awe na afya njema na uwezo wa kufanya kazi katika eneo na mazingira yoyote.
- i) Aambatishe picha mbili (2) za passport size.

## KAZI NA MAJUKUMU

- (i) Kukusanya na kuingiza taarifa za wamiliki wa Nyumba, Viwanja na Maeneo ya huduma kwenye mfumo wa Anwani za Makazi.
- (ii) Kutuma taarifa (Data) kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi kwa kila siku.

Mwombaji ahakikishe kwamba barua ya maombi imepitishwa na Mtendaji wa Kijiji pamoja na Mtendaji wa Kata anayokaa.

**Mwisho wa maombi haya ya ajira za muda ni tarehe 21/3/2022 saa 9:30 alasiri.**

**Mwombaji atume maombi kwa:-**

Mkurugenzi Mtendaji (W)  
Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi,  
S.L.P 20,  
**MISUNGWI.**

Imetolewa na:-

  
Leokadia G. Humera

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA  
MISUNGWI**

**NAKALA:** : Tovuti ya Halmashauri ya Misungwi - ([www.misungwidc.go.tz](http://www.misungwidc.go.tz))  
: Mbao zote za Matangazo